# Kutathmini athari za kimatamshi za kihaya kama lugha ya kwanza kwa wanaojifunza kiswahili sanifu kama lugha ya pili

**By**

**Godfrey Ndaluhela**

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**Email:** ndaluhelagodfrey@gmail.com

**Ikisiri**

*Utafiti huu ulitathmini athari za matamshi za Kihaya kama lugha ya kwaza kwa wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili. Wataalamu wengi wanakubaliana kuwa lugha zinapokutana huwa zinaathiriana. Utafiti ulifanyika katika mkoa wa Kagera katika wilaya ya Missenyi, Tanzania. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni hojaji na ushuhudiaji. Data za utafiti huu zimechanganuliwa kwa mkabala wa kimaelezo na kuongozwa na Nadharia ya Lugha Kadirifu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, kuna athari za uchopekaji wa fonimu, udondoshaji wa fonimu na kubadilisha fonimu. Aidha, Makala hii imeweka bayana mbinu zinazotumiwa na walimu kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya kujifunza Kiswahili sanifu ambazo ni kusoma kwa sauti, masahihisho kwa fonimu, nyimbo, kurudia rudia kutamka maneno, kutumia vielelezo na michoro na kuwapatia wanafunzi kazi za kutafuta maneno yenye silabi husika.*

***Maneno muhimu: Athari za matamshi, lugha ya Kihaya, lugha ya Kiswahili, sanifu***

## Utangulizi

Lugha ni sehemu muhimu katika maisha ya binadamu na katika jamii anamoishi. Hivyo palipo na watu huwepo pia lugha. Kimsingi lugha imebeba mambo mengi sana katika maisha ya binadamu. Suala la athari linajitokeza pale ambapo jamii mbili tofauti au zaidi zinazozungumza lugha tofauti zinapokaa pamoja na hapo panakuwepo na uwezekano mkubwa sana wa kuathiriana katika nyanja tofauti za kijamii na kiutamaduni (Obuchu na Mukhwana, 2015). Athari hii katika lugha hujitokeza katika matamshi, sarufi na hata lafudhi. Ipo mitazamo kinzani inayoeleza masuala ya athari ya L1 kwa wanaojifunza L2. Hope (2022) anasema kuwa, athari za

L1 katika L2 zinaweza kuwa hasi au chanya. Athari za L1 zinaweza kuwa chanya katika ujifunzaji wa L2 iwapo misingi na taratibu za L1 zimemsaidia anayejifunza L2 kuimudu katika matamshi sahihi. Cummins (1981) na Obondo (2001) wanasema kwamba, uwezo na weledi wa L1 huchangia pakubwa katika kujifunza L2. Kaoo na Upor (2021) wanasema kuwa, katika kujifunza L2 ni lazima L1 iwe na mchango wowote wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki.

Vile vile, athari za L1 zinaweza kuwa hasi iwapo misingi na taratibu za L1 zinamzuia mtu anayejifunza L2 asiwe na weledi fasaha katika L2. Dulay na wenzake (1982) wanadai kuwa, wakati mtu anajifunza L2 hukabiliwana matatizo fulani yakiwemo yale ya kushindwa kutamka kwa ufasaha na kushindwa kufuata muundo unaokubalika katika lugha husika. Wanaendelea kusisitiza kuwa, athari hizo zinaweza kuwa zinasababishwa na L1 ama mwalimu wa L2 kutokana na kutokuwa na weledi katika lugha hiyo. Kwa mujibu wa Richards (1974), tajriba ya mwanafunzi katika L1 huhamishiwa katika L2 kwa lengo la kurahisisha ujifunzaji wake. Uhamishaji wa aina hii husababisha kuwapo kwa makosa mbalimbali hususani iwapo mifumo ya lugha mbili husika ni tofauti. Lott (1983) amesema kwamba, makosa ambayo wanafunzi wa L1 wanayofanya yanatokana na L1.

Kwa mujibu wa sarufi majumui ni kuwa, sifa za lugha huingiliana; hivyo mwingiliano wa L1 na L2 unaweza kumwezesha muamiliaji wa L2 pale miundo ya L1 na L2 inapotofautiana na hata inapotofautiana anayejifunza anakuwa na uwezo wake wa kujiundia miundo yake itakayomsaidia

katika ujifunzaji wake. Flym (1984) akinukuliwa na Ellis (1996) anaeleza kuwa, kifaa (LAD) cha uamiliaji wa L1 kinaweza kutumika katika uamiliaji wa L2. Kifaa hiki siyo kifaa ambacho kinaweza kuguswa wala kuonwa bali ni kifaa ambacho ubongo wa mwanadamu huzaliwa nacho.

Pia, uwepo wa mitazamo kinzani juu ya athari za L1 katika kujifunza L2 ni sababu ya kufanyika kwa utafiti huu, wapo watafiti wanaodai kuwa ugumu wa uamiliaji L2 upo kwenye lugha lengwa yenyewe. Kwa mfano, Hussain (2023) anadai kuwa, katika kujifunza lugha lengwa lazima L1 itumike kumwongezea uelewa na kumwondolea woga anayejifunza lugha lengwa. Anaendelea kusisitiza kuwa, lugha lengwa inapaswa kuongezewa matumizi na kupunguza matumizi ya L1 kwa sababu mwalimu atafundisha kwa lugha lengwa na atafsiri kwa L1. Kaoo na Upor (2021) wanasema kuwa, mwanafunzi huhusianisha maana ya msamiati ya lugha lengwa kwa kurejelea maana kutoka katika L1. Vilevile, wapo watafiti wengine wanaodai kuwa, L1 ni daraja au msaada katika kujifunza L2. Al-Musawi (2014) anasema kwamba, wanafunzi wanapokuwa

darasani wanapaswa kuruhusiwa kutafsiri L2 katika L1 ili kuwasaidia kujifunza kwa ufasaha. Pia, watafiti wengine hudai kuwa, L1 ni chanzo cha makosa katika kujifunza L2. Hili sintofahamu inahitaji njia za utafiti zenye uhakika na makini ili kufikia matokeo sahihi na ya kuaminika kuhusu athari za L1 katika kujifunza L2.

Utafiti huu umetathmini athari za kimatamshi kwa wazungumzaji wa Kihaya kama L1 wanaojifunza Kiswahili sanifu kama L2. Kwa mujibu wa wataalamu na watafiti mbalimbali wa masuala ya lugha, L1 ni lugha ambayo mtu anajifunza kwanza maishani mwake kabla ya lugha nyingine. Hata hivyo, ni vigumu sana kwa jamii moja kutumia lugha moja katika mawasiliano hasa jamii hiyo inapokutana na jamii inayozungumza lugha nyingine tofauti. Katika mazingira kama haya, kunakuwepo na uhitaji wa mzungumzaji wa L1 kujifunza L2. Kutokana na hoja hizo, utafiti huu ulizingatia mtazamo wa kuwa L1 ni kikwazo na chanzo cha makosa kwa wale wanaojifunza L2. Uwepo wa athari za kifonolojia kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

## Mapitio ya kazi tangulizi

### Athari za Lugha Mama kwa Waamiliaji wa L2

Mudhune (1994) alichunguza ujifunzaji wa mofosintaksia ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiluo kwa mtazamo wa uchanganuzi linganuzi. Aligundua kuwa, makosa kadha yaliyojitokeza katika kazi za wanafunzi husika yalitokana na athari za lugha yao ya kwanza (Kiluo). Hata hivyo, alisisitiza kuwa, kulikuwa na makosa mengine yaliyogunduliwa na ambayo hayakuwa na chanzo chake katika lugha ya kwanza iliyotumiwa na wanafunzi waliochunguzwa. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kujua kuwa mbali na athari L1 katika kujifunza L2 zipo sababu nyingine zinazosababisha athari katika kujifunza L2 ambazo ni pamoja na mbinu zinazotumiwa na walimu kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili Sanifu.

Komunte (2001) alitathmini athari ya lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania. Anaeleza kuwa, mazingira ya darasani yalitawaliwa na wingi-lugha ambapo wanafunzi wote waliochunguzwa walikuwa wakitumia lugha mbalimbali za Kibantu kama lugha zao za kwanza. Hali hii, kwa mujibu wa utafiti alioufanya Komunte, ilichangia kwa sehemu kubwa ugumu uliodhihirika katika ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi husika. Kwa mujibu wa Komunte, alichangia kwa sehemu kubwa ugumu uliodhihirika katika ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi husika. Kwa mujibu wa mchunguzi huyu, asilimia 82.9 ya wanafunzi walikiri kuwa,

katika ujifunzaji wa stadi za kuzungumza na kusoma, walifikiria kwanza katika lugha ya kwanza na kisha kuwasilisha dhana husika katika lugha ya kujifunzia yaani Kiingereza. Mtaalamu huyo aligundua pia kwamba, wanafunzi wengi hawakuwa na umilisi wa msamiati wa Kiingereza huku wengine wakitamka maneno ya Kiingereza kama yalivyoandikwa. Aidha, huku akitoa mifano ya fonimu mbalimbali za Kiingereza zilizotamkwa kwa njia isiyo sahihi, anabainisha kuwa, lugha ya kwanza ya mwanafunzi husika ndiyo iliyochangia katika matamshi yasiyo sahihi. Akishughulikia suala la athari za kitigania kama L1 kwa wanaojifunza Kiswahili kama L2, Mukuthuria (2004), alibaini ya kwamba, kuna matatizo mengi ya kiisimu yanayowakumba wanafunzi wanaotumia lugha ya Kitigania wanapojifunza Kiswahili. Matatizo anayoyataja ni pamoja na yale ya kitahajia, kisarufi, uchanganyaji ndimi na kutafsiri dhana za Kiswahili kwa misingi ya kitigania. Uchunguzi uliofanywa na mwanataaluma huyu ulithibitisha kwamba, chanzo cha matatizo hayo ni mifumo ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha hizi. Akishughulikia kuibuka kwa 'Viswahili' na utafiti wa Kiswahili, Munyua (2002) anasema kuwa, athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi. Anaitumia dhana ya 'Viswahili' kurejelea matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili kutokana na uhamishaji hasi kutoka kwa lugha mbalimbali za kwanza kama vile: Kibukusu, Kikisii, Kikikuyu, Kimeru, Kikalenjin na Kiluo. Alisisitiza kuwa athari husika hujitokeza katika viwango vyote vya lugha ambavyo ni: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kuhusu idadi ya makosa katika tamko, Munyua alishikilia kuwa, iwapo makosa ni mengi, tamko husika hukanganya; hivyo kutoeleweka. Mudhune (2008) alichunguza athari za kifonolojia kwa wasemaji wa Kiluo wanaojifunza Kiswahili. Aligundua kwamba, kutofautiana kwa Kiswahili na Kiluo kifonolojia, kulisababisha makosa katika kipengele husika. Alieleza kuwa, wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama L2, wanafunzi wazawa wa Kiluo waliingiza kanuni za lugha yao ya kwanza katika Kiswahili. Athari kubwa ya kifonolojia aliyogundua mtafiti huyu, ilihusisha sauti ambazo zinapatikana katika L2 lakini zisizopatikana katika L1. Ontieri (2010) alitafiti athari za kifonolojia za L1 katika Kiswahili. Mtafiti huyu alitumia mifano ya lugha za Kibantu kutoka nchini Kenya. Katika utafiti wake aligundua kuwa, lugha za Kibantu ni kikwazo katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu ambapo mtafiti alionesha kuwa, wazungumzaji wa Kibantu nchini kwenye hufanya makosa ya udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu. Katika uchopekaji mtafiti anaonesha kuwa, irabu /u/ huchopwekwa katikati ya konsonanti mbili. Kwa mfano: kutamka /kuamuka/ badala ya /kuamka/, katika udondoshaji sauti nazali zilidondoshwa katika sauti mwambatano, walitamka /majozi/ badala ya /majonzi/ na katika ubadilishaji wa fonimu, mtafiti alionesha wanafunzi walitumia sauti /g/ badala ya /gh/ na sauti /s/ badala ya /sh/.

Wenceslaus (2015) alitafiti athari za lugha ya Kijita katika kujifunza Kiswahili. Katika utafiti wake aligundua kuwa, Wajita huathiri uamiliaji wa Kiswahili kwa kufanya udondoshaji wa baadhi ya sauti. Kwa mfano, sauti /h/ ambapo husema /ataki/ badala ya /hataki/. Pia aligundua kuwa, Wajita hutumia sauti /z/ badala ya /dh/, sauti /s/ badala ya /th/ na sauti /g/ badala ya /gh/. Naye Mpangala (2018) alitafiti athari za lugha ya Kimakonde katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Aligundua kuwa, Wamakonde hutumia sauti mbadala wakati wanapotamka maneno ya Kiswahili. Mtafiti huyu aling'amua kuwa, athari za kimatamshi zinatokana na ndimi za wahusika kuathiriwa na Kimakonde na kusababisha kukosekana kwa baadhi ya sauti kama vile /m/, /r/, /ʃ/, /ð/, /ɵ/, /z/ na /h/.

## *2.2* Sababu za L1 Kuathiri Uamiliaji wa L2

Bartoo (2004), akichunguza ujifunzaji wa sintaksia ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaotumia Kikeiyo kama L1 na aligundua kuwa, Kikeiyo kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiingereza. Anasema kwamba, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizo mbili, wanafunzi husika walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao hadi kuwa katika lugha ya Kiingereza. Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyoyabainisha mtafiti huyu katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa hao. Edward (2011) alichunguza makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa Kikamba wanapojifunza Kiswahili sanifu. Katika matokeo ya utafiti wake alionesha wazi kwamba, wanafunzi wanafanya makosa kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisimu ya lugha yao ya kwanza na kulazimisha mifumo hiyo katika kujifunza Kiswahili sanifu. Badala yake wanaishia kufanya makosa na kuibua lugha ya kati. Edward (ameishatajwa) anaendelea kufafanua kuwa, makosa yanatokana na ujumuishaji mno wa kanuni za lugha za L1. Katika lugha ya Kikamba kuna kanuni ya kutanguliza kila neno na fonimu za nazali wanachukulia hivyo pia katika Kiswahili sanifu. Nyanda (2015) alichunguza athari za lugha ya Kinyamwezi kwa wanaojifunza Kiswahili. Alibaini kuwa, kukosekana kwa baadhi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kinyamwezi husababisha wazungumzaji wa Kinyamwezi kutumia msamiati wa Kinywamwezi wakati wa kujifunza Kiswahili. Kanake (2013) alichunguza makosa ya kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kigembe katika ujifunzaji wa Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa, chanzo cha athari ni tofauti katika mifumo ya lugha ya Kigembe na Kiswahili ambapo Kigembe kilikuwa na takribani konsonanti 13 wakati lugha ya Kiswahili ilikuwa na konsonanti 25. Sababu kama hii ilitajwa na Nyanda (2015) wakati akichunguza athari za lugha ya Kinyamwezi kwa wanaojifunza Kiswahili. Nyanda (ameishatajwa) anasema kuwa sababu ya lugha ya Kiswahili kuathiriwa na

Kinyamwezi katika viwango vyote vya kiisimu kuwa ni kukosekana kwa sauti /r/, /gh/, /th/, /dh/ na /b/ katika lugha ya Kinyamwezi. Edward (2011) anataja sababu ya kuwa walimu ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kigembe wana utendaji mbaya katika uzungumzaji wa Kiswahili na hivyo wanafunzi nao pia wanachukulia hivyo hivyo. Kanake (2013 anasema kuwa, wanafunzi walifanya makosa kwa sababu hawana umilisi wa lugha ya Kiswahili. Nyanda (2015) alibaini kuwa, ufundishaji mbaya wa walimu wa lugha ya Kiswahili na wanafunzi kutopata muda wa kutosha kujifunza na kuzungumza Kiswahili wawapo nje ya mazingira ya shule na wazazi wao kutokuona umuhimu wa lugha ya Kiswahili na somo la Kiswahili ni sababu zinazosababisha Kinyamwezi kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.maelezo ya wataalamu hawa yalimsaidia mtafiti kujua sababu za L1 kuathiri uamiliaji wa L2.

**Mbinu na njia za utafiti**

Utafiti huu ulitumia hojaji na ushuhudiaji kama mbinu ya kukusanya data kutoka kwa watafitiwa. Mtafiti alipanga data kutokana na maudhui na makundi ya wasailiwa yanayofanana kisifa. Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki na kutafsiri data alizozipata katika utafiti huu kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki na kupanga data katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Data za aina moja ziliwekwa pamoja ili kurahisisha usomaji wa maudhui yaliyokusudiwa. Mkabala mmoja ulitumika katika ukusanyaji na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Mkabala huyo ni mkabala wa kimaelezo. Mkabala wa kimaelezo ulitumika pasipo kufuata taratibu za kitakwimu katika kutathmini athari za kimatamshi ya Kihaya kama L1 kwa wanaojifunza Kiswahili kama L2. Mkabala huu ulitumia majedwali kuonesha data ambazo zilifupishwa kwa namna ambayo ni rahisi kuchambuliwa na kueleweka kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

**Sampuli**

Katika utafiti huu usampulishaji wa makusudi ulitumika kupata watafitiwa. Sampuli katika utafiti huu ilikuwa watu 72 walimu 12 na wanafunzi 60) ambapo kila shule ilitoa walimu wawili (2) ambao ni mahiri katika utamkaji wa sauti za lugha ya Kiswahili na Kihaya na wanafundisha somo la Kiswahili katika darasa tatu na darasa la nne. Walimu walichaguliwa kwa sababu hukutana na makosa ya kimatamshi mara kwa mara wakati wa kusahihisha kazi andishi za wanafunzi. Kupitia sampuli hii, mtafiti alipata taarifa za malengo yake yote matatu ya utafiti ambayo ni kubainisha makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza kiswahili sanifu. Vile vile, kubainisha sababu za wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa katika kujifunza Kiswahili sanifu. Pia, kubainisha mbinu za kutumia ili

kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili. Sampuli ya pili katika utafiti huu ilikuwa ni ya wanafunzi 60 wa darasa la tatu na la nne wanaozungumza Kihaya na hivi sasa wanajifunza Kiswahili sanifu. Ambapo kila darasa lilikuwa na wanafunzi 50 ambapo kwa kutumia usampulishaji wa makusudi watafitiwa 10 ndiyo waliyotumika katika utafiti huu yaani darasa la tatu lilitoa wanafitiwa 5 na darasa la nne watafitiwa 5 kwa kila shule. Watafitiwa hawa ni wale ambao lugha yao ya kwanza ni Kihaya. Idadi ya watafitiwa hawa ilipatikana kwa kutumia usampulishaji wa makusudi ili kuhakikisha kuwa watafitiwa wote ni wazungumzaji wa lugha ya Kihaya na hivyo wanajifunza Kiswahili kama L2. Mtafiti alichagua sampuli hii kwa sababu wao ndiyo hutenda makosa ya kimatamshi wakati wa kuongea na kuandika Kiswahili sanifu. Hivyo, sampuli hii ilimsaidia mtafiti kupata taarifa za lengo la kubainisha makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Mtafiti aliteua sampuli ya utafiti kulingana na sifa ya kuwa wana uwezo wa kutoa data sahihi zilizotakiwa kulingana na lengo la utafiti huu yaani watakaokuwa na uwezo wa kutoa habari faafu zilizojibu kikamilifu maswali ya utafiti. Katika utafiti huu, watafitiwa 72 waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa (wa makusudio).

**Jedwali 1: Mchanganuo wa Sampuli**

| Na. | Kundi la sampuli | Idadi ya watafitiwa |
|---|---|---|
| **1.** | Wanafunzi wa shule za msingi | 60 |
| **2.** | Walimu | 12 |

Aina ya hojaji iliyotumika katika utafiti huu ilijumuisha aina zote mbili za maswali yaliyokuwemo katika hojaji, maswali funge na maswali yasiyofunge. Mtafiti aliamua kuchanganya aina zote za maswali ili kuepuka kasoro zinazoweza kutokea katika aina hizi mbili, ikizingatia kuwa kila moja ina kasoro zake. Hivyo, aina hizo zilitumika kwa pamoja ili kukamilishana. Mtafiti aliwapa watafitiwa wake ambao ni walimu hojaji wajaze papo kwa papo na kisha warejeshe kwa ajili ya uchambuzi wa data. Njia ya hojaji ilichaguliwa kwa sababu inafaa kukusanya data nyingi kwa muda mfupi sana hasa hojaji za papo kwa papo. Aidha, ni njia rahisi na ya haraka katika kukusanya na kuchanganua data. Data zilizopatikana kwa njia hii zilimsaidia mtafiti kupata taarifa ya lengo lake ambayo ni kubainisha athari za kimatamshi za Kihaya kama L1 kwa wanaojifunza Kiswahili sanifu kama L2.

## Uwasilishaji na uchambuzi wa data

### Utangulizi

Sura hii ni ya uwasilishaji wa data za kutathmini athari za kimatamshi ya Kihaya kama Lugha ya kwanza kwa wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya pili. Data za utafiti huu zimekusanywa nyanjani kwa kutumia njia kuu mbili ambazo ni hojaji na ushuhudiaji. Data hizi zilikusanywa kutokana na sampuli ya wanafunzi wa darasa la nne na la tatu na walimu wanaofundisha madarasa hayo ambao wanaozungumza lugha ya Kihaya na Kiswahili sanifu kutoka shule ya msingi Bugandika 1, Bugandika 2, Kijumo, Kigarama, Kikukwe na Bugombe.

Uwasilishaji wa matokeo ulifanyika kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Lugha Kadirifu ambayo ilitathmini athari za kimatamshi za Kihaya kama L1 kwa wanaojifunza Kiswahili kama L2. Uwasilishaji wa matokeo haya ulilenga kujibu maswali ya utafiti ili kukamilisha malengo ya utafiti. Aidha, sura hii inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa data zilizochambuliwa na hoja mbalimbali za wataalamu kama zilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi za tutafiti huu.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili, ambazo ni:-

i. Athari za kimatamshi zinazofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.
ii. Sababu zinazosababisha Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu.

### Athari za Kimatamshi Zinazofanywa na Wazungumzaji wa Kihaya Wanaojifunza Kiswahili Sanifu

Katika kipengele hiki, mtafiti aliweza kubainisha athari za kimatamshi zinazofanywa na wazungumzaji wa Kihaya kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kama L2. Mtafiti aliweka bayana vikwazo vya kimatamshi ambavyo huwakumba wazungumzaji wa Kihaya wanapojifunza Kiswahili sanifu. Katika kubainisha athari za kimatamshi mtafiti alitumia mbinu ya hojaji ambazo alizigawa kwa walimu. Vile vile mtafiti alibainisha athari hizo kwa kutumia mbinu kushuhudia ambayo aliitumia kwa watafitiwa ambao ni wanafunzi.

**Jedwali 4.1: Majibu ya Hojaji ya Walimu juu ya Athari za Kimatamshi za Wazungumzaji wa Kihaya Wanaojifunza Kiswahili Sanifu**

| Na. | Kosa | Lipo | Halipo |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuchanganya sauti /ɵ/ na /s/ | 7 | 5 |
| 2 | Kuchanganya sauti /ð/ na /z/ | 9 | 3 |
| 3 | Kuchanganya sauti /gh/ na /g/ | 9 | 3 |
| 4 | Kuchanganya sauti /ŋ/ na /ng/ | 9 | 3 |
| 5 | Kuchopeka sauti irabu kwenye silabi funge. Kwa mfano kutamka /dafutari/ badala ya /daftari/ au /dakitari/ badala ya /daktari/ | 11 | 1 |
| 6 | Kuchanganya sauti /r/ na /l/ | 12 | 0 |
| 7 | Udondoshaji wa sauti /h/ katika neno. Kwa mfano, kutamka /eshima/ badala ya /heshima/ | 10 | 2 |
| 8 | Kuchopeka sauti /h/ katika neno. Kwa mfano, kutamka /msahada/ badala ya /msaada/ | 9 | 3 |
| 9 | Udondoshaji wa irabu katika neno. Kwa mfano, kutamka /mziki/ badala ya /muziki/ au /mda/ badala ya /muda/ | 11 | 1 |
| 10 | Kuchanganya sauti irabu /a/ na sauti konsonanti /w/. kwa mfano, kutamka / kua/ badala ya /kuwa/ | 8 | 4 |

Katika sehemu hii ya hojaji ya walimu, jumla ya walimu 12 walihusika kujaza hojaji ili kuonesha kama athari ipo au haipo kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Kipengele cha kwanza, watafitiwa 7 (58.3%) walionesha kuwa, kuna athari ya kuchanganya sauti /ɵ/ na /s/ wakati wazungumzaji wa Kihaya wanapojifunza Kiswahili sanifu. Watafitiwa 5 (41.7%) walionesha kuwa, hakuna athari ya kuchanganya sauti /ɵ/ za /s/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama L2 kwao.

Katika kipengele cha pili, watafitiwa 9 (75%) walionesha kuwa, ipo athari ya kuchanganya sauti /ð/ na /z/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Watafitiwa 3 (25%) walionesha kuwa, hakuna athari ya kuchanganya sauti /ð/ na /z/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Kipengele cha tatu, watafitiwa 9 (75%) walionesha kuwa, ipo athari ya kuchanganya sauti /gh/ na /g/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Watafiti 3 (25%) walionesha kuwa, hakuna athari ya kuchanganya sauti /gh/ na /g/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Kipengele cha nne, watafitiwa 9 (75%) walionesha kuwa, ipo athari ya kuchanganya sauti /Ŋ/ na /ng/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza

Kiswahili sanifu. Watafiti 3 (25%) walionesha kuwa, hakuna athari ya kuchanganya sauti /Ŋ/ na /ng/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Kipengele cha tano, watafitiwa 11 (91.6%) walionesha kuwa, kuna uchopekaji wa irabu kwenye silabi funge kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Mtafitiwa 1 (8.4%) alionesha kuwa, hakuna uchopekaji wa sauti irabu kwenye silabi funge kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Kipengele cha sita, watafitiwa 12 (100%) walionesha kuwa, ipo athari ya kuchanganya sauti /r/ na /l/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Katika kipengele hiki, hakuna mtafitiwa hata mmoja aliyeonesha kuwa, hakuna athari ya kuchanganya sauti /r/ na /l/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Katika kipengele cha saba, watafitiwa 10 (83.3%) walionesha kuwa, ipo athari ya udondoshaji wa sauti /h/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Watafitiwa 2 (16.7%) walionesha kuwa, hakuna athari ya udondoshajiwa sauti /h/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Kipengele cha nane, watafitiwa 9 (75%) walionesha kuwa, ipo athari ya uchopekaji wa sauti /h/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Watafitiwa 3 (25%) walionesha kuwa, hakuna uchopekaji wa sauti /h/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Kipengele cha tisa, watafitiwa 11 (91.6%) walionesha kuwa, ipo athari ya kudondosha sauti irabu katika maneno kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Mtafitiwa 1 (8.4%) alionesha kuwa, hakuna udondoshaji wa sauti irabu katika maneno kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Kipengele cha kumi, watafitiwa 8 (66.6%) walionesha kuwa, ipo athari ya kuchanganya sauti irabu /a/ na sauti konsonanti /w/ kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Watafiwa 4 (43.4%) walionesha kuwa, hakuna athari ya kuchanganya sauti irabu /a/ na sauti konsonanti /w/ kwa wazungumzaji wa wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

**Athari za Kimatamshi Zilizofanywa na Wazungumzaji wa Kihaya Wanaojifunza Kiswahili Sanifu Zilizokusanywa kwa Njia ya Kushuhudia**

Mtafiti alitumia njia ya kushuhudia katika ukusanyaji wa data za utafiti wake ambapo mtafiti alishuhudia namna wazungumzaji wa Kihaya walivyokuwa wakitamka maneno ya Kiswahili sanifu. Kupitia njia ya kushuhudia, mtafiti aliweza kubainisha athari za kimatamshi zinazofanywa na wazungumzaji wa Kihaya kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kama L2. Mtafiti alibainisha kuwa, wazungumzaji wa lugha ya Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu hukumbana na vikwazo vifuatavyo wakati wa kutamka maneno ya Kiswahili sanifu.

**Udondoshaji wa Fonimu**

Kwa mujibu wa Ontieri (2010), odondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti katika uundaji wa maneno katika lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili zilisababisha kuondoshwa kwa sauti irabu na sauti konsonanti kwa njia inayoleta kasoro katika maneno mbalimbali. Makosa ya udondoshaji yaliyoshuhudiwa katika mazungumzo ya Wahaya wanaojifunza Kiswahili sanifu yapo kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.2: Mifano ya Udondoshaji wa Fonimu**

| Na. | Udondoshaji | Sahihi |
|---|---|---|
| 1 | Apana | Hapana |
| 2 | Eshima | Heshima |
| 3 | Gorofa | Ghorofa |
| 4 | Mda | Muda |
| 5 | Mziki | Muziki |

Mtafiti alishuhudia udondoshaji wa sauti /h/ na irabu /u/ katika maneno ya lugha ya Kiswahili sanifu. Wazungumzaji wa lugha ya Kihaya hutamka sauti /h/ kama wanavyotamka sauti irabu /a/, /e/, /i/, /o/ na /u/. Sauti irabu hutamkwa huku kikiwa hakuna kuzuiliwa kwa hewa kutoka kwenye mapafuhadi kwenye kinywa na utamkwaji wa sauti irabu huzingatia mkaowa mdomo, hali ya ulimi na sehemu ya ulimi iliyoiuka. Wakati sauti /h/ hutamkiwa katika kwenye koromeo wakati koromeo limefunguliwa. Vile vile, mtafiti alishuhudia watafitiwa wakifanya makosa ya

udondoshaji wa sauti irabu /u/ pale inapotanguliwa na konsonanti ya nazali /m/ na kusababisha silabi hiyo kutamkwa kwa makosa.

### Uchopekaji wa Fonimu

Ontieri (2010) anasema kwamba, uchopekaji ni mchakato wa kifonolojia unaorejelea hali ambapo kipashio huongezwa katika neno. Matokeo yake ni kuzalisha neno lenye sauti ya ziada ambayo haipo katika neno la msingi. Makosa ya uchopekaji ambayo mtafiti aliyashuhudia katika mazungumzo ya Wahaya wanaojifunza Kiswahili sanifu yalijitokeza katika mifano ya maneno yafuatayo:

**Jedwali 4.3: Mifano ya Uchopekaji wa Fonimu**

| Na. | Uchopekaji wa fonimu | Sahihi |
|---|---|---|
| 1 | Msahada | Msaada |
| 2 | Rahia | Raia |
| 3 | Habiria | Abiria |
| 4 | Asikari | Askari |
| 5 | Dafutari | Daftari |
| 6 | Elufu | Elfu |
| 7 | Afirika | Afrika |

Mtafiti alishuhudia wanafunzi katika mazungumzo yao wakifanya makosa ya uchopekaji wa sauti /h/ na sauti irabu /i/ na /u/. Uchopekaji wa sauti /h/ ulitokea kabla ya irabu. Hivyo, wanafunzi hawakujua sauti /h/ inafaa kutumika wakati gani.

Vile vile, sauti irabu /i/ na /u/ zilichopekwa katika silabi funge. Kwa mujibu wa Matinde (2012), silabi funge ni silabi ambazo huishia kwa konsonanti. Katika maneno ya Kiswahili sanifu ambayo yana silabi funge, mtafiti alibainisha wanafunzi walichopeka sauti irabu /i/ au /u/ na kuunda neno lenye makosa katika matamshi.

### Kubadilisha Fonimu

Makosa yaliyojitokeza katika kipengele hiki yalihusu matumizi ya fonimu fulani ambapo fonimu nyingine iliyosahihi ilistahili kutumiwa. Mtafiti alishuhudia mazungumzo ya wanafunzi yakifanyika huku wakibadilisha fonimu katika baadhi ya maneno. Sauti hizo zilizoshuhudiwa zikibadilishana nafasi zipo kama ifuatavyo:

**Fonimu /ŋ/ kubadilishwana fonimu /ng/**

Katika lugha ya Kihaya, fonimu /ng'/ haipo badala yake wanafunzi walioshuhudiwa walitumia fonimu /ng/ kama mbadala wakati wa kuzungumza Kiswahili sanifu. Mifano ya maneno iliyobainishwa kwa kutumia njia ya kushuhudia ipo kama ifutavyo:

**Jedwali 4.4: Mifano ya sauti /ŋ/ Kubadilishwa na fonimu /ng/**

| **Na.** | **fonimu Iliyobadilishwa** | **Fonimu Sahihi** |
|---|---|---|
| 1 | Ngombe | Ng'ombe |
| 2 | Ngoa | Ng'oa |
| 3 | Ngaa | Ng'aa |

**Fonimu /gh/ Kubadilishwa na fonimu /g/**

Fonimu /gh/ haipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya ila ipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kiswahili. fonimu /g/ ipo katika mfumo wa lugha zote mbili yaani lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili. Kwa wanafunzi walioshuhudiwa katika mazungumzo yao, walibadilisha fonimu /gh/ na kuwa fonimu /g/. Mifano ya kubadilishwa kwa fonimu iliyoshuhudiwa ipo kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.5: Mifano ya sauti /gh/ Kubadilishwa na fonimu /g/**

| **Na.** | **fonimu Iliyobadilishwa** | **fonimu Sahihi** |
|---|---|---|
| 1 | Gorofa | Ghorofa |
| 2 | Luga | Lugha |
| 3 | Shuguli | Shughuli |

Mtafiti alibaini kuwa fonimu /gh/ na /g/ hutamkiwa kwenye kaakaa laini, hivyo wanafunzi walioshuhudiwa walionekana kutaka kurahisisha mfumo wa sauti za lugha lengwa. Matokeo yake, neno lilitamkwa kimakosa na kutengeneza fonimu isiyo sahihi.

**Fonimu /ɵ/ Kubadilishwa na fonimu /s/**

Mtafiti alishuhudia wanafunzi wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu wakitumia fonimu /s/ badala ya fonimu /ɵ/. Mtafiti alibaini kuwa, katika mfumo wa sauti za

lugha ya Kihaya hakuna fonimu /th/ badala yake kuna fonimu /s/ ambayo ina ufanano wa karibu sana kimatamshi na fonimu /ɵ/. Mifano ya kubadilishwa kwa fonimu iliyoshuhudiwa ipo kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.6: Mifano ya fonimu /ɵ/ Kubadilishwa na fonimu /s/**

| Na. | fonimu Iliyobadilishwa | fonimu Sahihi |
|---|---|---|
| 1 | Asari | Athari |
| 2 | Samani | Thamani |
| 3 | Tasimini | Tathmini |

Fonimu /s/ na /ɵ/ zina sifa zinazofana kifonolojia ambapo fonimu hizi ni vikwamizo si ghuna. Hivyo, katika mfumo wake wa ufundishaji wanafunzi huweza kuzifananisha kimatamshi. Matokeo yake ni kuunda maneno mengine yenye maana tofauti na iliyokusudiwa au isiyokuwepo katika lugha ya Kiswahili.

**Fonimu /ð/ Kubadilishwa na fonimu /z/**

Kwa kutumia njia ya kushuhudia, mtafiti alishuhudia wanafunzi walitamka fonimu /z/ badala ya /ð/. Hii ni kutokana na fonimu /ð/ kutokuwa katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya.

**Jedwali 4.7: Mifano ya sauti /ð/ Kubadilishwa na sauti /z/**

| Na. | fonimu Iliyobadilishwa | fonimu Sahihi |
|---|---|---|
| 1 | Baazi | Baadhi |
| 2 | Zambi | Dhambi |
| 3 | Zaifu | Dhaifu |

Wakati wa mazungumzo yao, wanafunzi walishindwa kutamka maneno yaliyokuwa yana fonimu /ð/ na badala yake walitamka /z/ na kuunda maneno ambayo hayapo katika lugha ya Kiswahili sanifu.

**Sababu Zinazosababisha Kihaya Kuathiri Uamiliaji wa Kiswahili Sanifu**

Kipengele hiki kimebainisha sababu zinazosababisha wazungumzaji wa Kihaya kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Sababu hizo zilikusanywa nyanjani kwa kutumia njia ya hojaji ambapo watafitiwa 12 ambao ni walimu walihusika. Katika kukusanya data za kipengele hiki

mtafiti aliainisha sababu na kuwataka watafitiwa wakubali kuwa ni sababu ya Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu au wakatae kuwa siyo sababu inayosababisha Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu au mtafitiwa aoneshe hana uhakika na sababu hiyo. Data za sababu zinazosababisha Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu zimeainishwa katika jedwali 4.8 hapo chini.

**Jedwali 4.8: Sababu Zinazosababisha Kihaya Kuathiri Uamiliaji wa Kiswahili Sanifu**

| Na | Sababu za kufanya makosa | Nakubaliana | Nakataa | Sina uhakika |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tofauti za Kimuundo kati ya kugha ya Kihaya na Kiswahili | 8 | 3 | 1 |
| 2 | Kuhamisha mifumo ya ya Kimatamshi ya lugha ya Kihaya na kuitumia katika Kiswahili | 10 | 1 | 1 |
| 3 | Utamkaji mbaya wa baadhi ya maneno kutoka kwa walimu wao | 5 | 4 | 3 |
| 4 | Matumizi ya Kihaya muda mwingi wawapo katika mazingira ya shule na nyumbani. | 9 | 1 | 2 |
| 5. | Matumizi ya mbinu zisizofaa za ufundishaji wa lugha ya pili. | 6 | 4 | 2 |

Katika kipengele cha kwanza, mtafiti alitaka kujua kama tofauti za kimuundo kati ya lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa sababu ya Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu. Kipengele hiki kilihusisha jumla ya watafitiwa 12 ambao ni walimu ambapo watafitiwa 8 (66.7%) walikubali, watafitiwa 3 (25%) walikataa na mtafitiwa 1 (8.3%) hakuwa na uhakika. Komunte (2001) wanafunzi wengi hawakuwa na umilisi wa msamiati wa Kiingereza huku wengine wakitamka maneno ya Kiingereza kama yalivyoandikwa. Katika kipengele cha

pili, mtafiti alitaka kubaini kama kuhamisha mifumo ya kimatamshi ya lugha ya Kihaya na kuitumia katika Kiswahili inaweza kuwa sababu ya lugha ya Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu. Edward (2011) katika lugha ya Kikamba kuna kanuni ya kutanguliza kila neno na fonimu za nazali wanachukulia hivyo pia katika Kiswahili sanifu. Watafitiwa waliohusika katika kipengele hiki ni 12 ambapo watafitiwa 10 (83.4%) walikubaliana, mtafitiwa 1 (8.3%) alikataa na mtafitiwa 1 (8.3%) hakuwa na uhakika. Kipengele cha tatu, mtafiti alitaka kubaini kama utamkaji mbaya wa baadhi ya silabi kutoka kwa walimu ni miongoni wa sababu za lugha ya Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu. Edward (2011) walimu ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kigembe wana utendaji mbaya katika uzungumzaji wa Kiswahili na hivyo wanafunzi nao pia wanachukulia hivyo hivyo. Jumla ya watafitiwa waliojaza hojaji katika kipengele hiki ni 12 ambapo watafitwa 5 (41.7%) walikubali, watafitiwa 4 (33.3%) walikataa na watafitiwa 3 (25%) hawakuwa na uhakika. Kipengele cha nne, mtafiti alitaka kubaini kama matumizi ya Kihaya muda mwingi wawapo katika mazingira ya shule na nyumbani inaweza kuwa sababu ya lugha ya Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu. Nyanda (2015) wanafunzi kutopata muda wa kutosha kujifunza na kuzungumza Kiswahili wakiwa nje ya mazingira ya shule na wazazi kutokuona umuhimu wa lugha ya Kiswahili na somo la Kiswahili ni sababu zinazosababisha Kinyamwezi kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Katika kipengele hiki jumla ya watafitiwa 12 walihusika ambapo watafitiwa 9 (75%) walikubali, mtafitiwa 1 (8.3%) alikataa na watafitiwa 2 (16.7%) hawakuwa na uhakika. Kipengele cha tano, mtafiti alilenga kubaini kama matumizi ya mbinu zisizofaa za ufundishaji wa lugha ya pili ni miongoni mwa sababu za lugha ya Kihaya kuathiri uamiliaji wa Kiswahili sanifu. Manyau (2002) alipendekeza kuwa tafiti nyingine zifanywe kuhusu Viswahili kwa lengo la kuwaelekeza watunga mitaala ya Kiswahili kuzua mbinu mpya za ufundishaji wa Kiswahili sanifu. Jumla ya watafitiwa walikuwa 12 ambapo watafitiwa 6 (50%) walikubali, watafitiwa 4 (33.3%) walikataa na watafitiwa 2 (16.7%) hawakuwa na uhakika.

## Hitimisho na mapendekezo

### Hitimisho

Kupitia kufanyika kwa utafiti huu, matokeo yake yamedhihirisha athari za matamshi ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Vile vile, sababu za Kihaya kuathiri uamiliaji wa lugha ya Kiswahili zimewekwa bayana kupitia utafiti huu.

### Mapendekezo

Mtafiti anapendekeza sehemu zifuatazo kushughulikiwa na tafiti zingine. Kwanza, kutathmini athari za vipengele vingine vya kiisimu mbali na athari za kimatamshi zichunguzwe. Pili, mbinu zaidi za kukusanya data zihuzishwe katika tafiti za usoni; matokeo yatakayotokana na mbinu hizo yanaweza kutumiwa kulinganisha matokeo ya utafiti huu uliotumia mbinu tatu. Tatu, sampuli za wanafunzi kutoka viwango tofauti tofauti zitumike kwa nia ya kulinganisha hatua za kujifunza lugha zao lengwa. Hali kadhalika, tafiti za jinsi hii zifanywe katika maeneo mbalimbali yenye L1 tofauti kwa minajili ya kulinganisha matokeo haya na hata kubaini ikiwa matokeo ya jinsi hii yana umajumui wowote kwa kila anayejifunza lugha ya pili.

**Marejeleo**


Al-Musawi, N. M. (2014). *Strategic use of translation in learning English as a foreign language (EFL) among Bahrain University students. Journal of Comprehensive.*

Bartoo, J. P. (2004). *Acquisition of English syntax by Keiyo L1 speakers*. (Tasnifu ya kutunukiwa shahada ya uzamili). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Cummins, J. (1981). *The role of primary language development in promoting educational success for language minority students.* A theoretical rationale. Calforniastate Department of Education

Dulay, H, Burt, M., & Krashen, S. (1982). *Language two.* Oxford of Univerity Press.

Edward, M. J. (2011). Uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kikamba wanaojifunza Kiswahili Sanifu. (Tasnifu ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ellis, R. (1997). *Second language acquisition*, Oxford University. Press.

Hope. (2022). *Athari za lugha mama katika ujifunzaji wa kiswahili kama lugha ya lili miongoni mwa wanafunzi waganda wanaojifunza Kiswahili.* (Mahitaji ya Shahada ya Sanaa na Elimu). Chuo Kikuu Makerere.

Hussain, S. S. (2023). *The influence of L1 in English language acquisition: A case study of ES learners at King Saud University*. Rupkatha  Journal. DI:10.33086/ehdj. V 3i1.89

Kanake, J. K. (2013).  *Makosa ya kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili.* (Tasnifu ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kaoo & Upor (2021). Lemmatic influence on vocabulary acquisition among L3 English language learners in Tanzania. Indonesia *Journal of Applied Linguistics*. DOI: https://doi.org/10.17509/ijal.v11i1.34671

Komunte, B. S. (2001). *The Impact of bantu languages in English language learning processes in Tanzania secondary schools.* Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili, 2000, 287 – 296.

Lott, D. (1983). Analysing and counteracting interference errors ELT. *Journal of Scholars Portal*, 37(3), 256-261.

Mpangala, G. (2018). *Athari ya lugha ya Kimakonde katika kujifunza lugha ya Kiswahili.* (Tasnifu ya Kutunukiwa Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria.

Mudhune, D. R. (2008). *Athari za kifonolojia kwa wasemaji wa dholuo wanaojifunza Kiswahili.* (Tasnifu ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili). Chuo Kiku cha Egerton, Kenya.

Mudhune, E. S. (1994). A constructive analysis approach to the learning of Swahili morphosyntax by Luo speakers. In Ontieri, J. O. (2013). *Phonological influenceof first languages on Kiswahili: A case study of Kenyan bantu languages*. Maasai Mara University. Kenya.

Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano Kutokana na Wanafunzi wa Kitigania, Kenya*. Tasnifu ya PhD Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Munyua, J. G. (2002). *The emerging Viswahili and Kiswahili research*. Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Moi University Press. Eldoret.

Obondo, I. B. (2007). *The American Journal on addictions, 20(2),* 87-99.

Ontieri, J. O. (2010). *Athari za kifonolojia za lugha ya kwanza katika Kiswahili. Mfano wa lugha teule za Kibantu Nchini Kenya.* https://journals.udsm.ac.tz.

Richards, J. C. (1974). *Errors analysis and second language strategies.* Paper presented at Midis du GREDIL, Université Laval, Sainte-Foy, Quebec: Canada.

Selinker, L. (1972). *Interlanguage*. Eribaum Associates. https://www.degruyter.com

Selinker, L. (1969). *Language Transfer. General Linguistics*. Eribaum Associates. New York Rawlence.

Wenceslaus, M. (2015). *Athari za lugha ya Kijita katika kujifunza Kiswahili.* (Tasnifu ya Kutunukiwa Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.